Kanuni ya Maadili ya Msambazaji

Katika kampuni la Fruit of the Loom na makampuni yetu tunayoshirikiana nayo ("FOTL"), tumejitolea kuendesha biashara kwa kuzingatia viwango vya juu zaidi vya maadili ya biashara na heshima kwa haki za binadamu na mazingira. Tunahitaji kujitolea sawa kutoka kwa vituo vyote vinavyosambaza bidhaa zetu, ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu, wakandarasi, wenye leseni na washirika wengine wa biashara walioteuliwa (kwa pamoja wanajulikana kama "Wasambazaji"). Kanuni hii ya Maadili ya Wasambazaji huonyesha viwango ambavyo tunahakikisha kwamba kujitolea huku kunatimizwa na Wasambazaji na kunaongozwa na kanuni kutoka kwa Mikataba ya Msingi ya Shirika la Kazi la Kimataifa na Kanuni ya Maadili ya Mahali pa Kazi ya Chama cha Kazi cha Haki.

INAYOZINGATIA-WATU

Uhusiano wa Kiajira: Wasambazaji watatumia na kufuata sheria na masharti ya ajira yanayoheshimu wafanyakazi na, na watalinda haki zao chini ya sheria na kanuni za kitaifa na za kimataifa za kazi na za usalama wa kijamii.

Afya na Usalama: Wasambazaji watatoa pahali salama na pazuri pa kufanyia kazi ili kuzuia ajali na majeraha yanayotokana na shughuli za Msambazaji. Hali katika kiwanda/kampuni nzima la Msambazaji, zikiwemo dahalia/bweni zinazomilikiwa au kuendeshwa na Msambazaji, lazima ziwe salama, safi na zitimize au zizidi mahitaji ya sheria na kanuni zote za usalama na afya zinazohusika. Wafanyakazi lazima wafundishwe na wapatiwe vifaa vinavyofaa ili waweze kufanya kazi zao kwa usalama.

Kuajiri Watoto: Wasambazaji hawatawaajiri watu ambao lazima waende shuleni au walio chini ya umri unaoruhusiwa kisheria. Hakuna wakati ambapo Wasambazaji watawaajiri wafanyakazi walio chini ya miaka 15, isipokuwa watoto wanaoigiza au wasanii wanaotumika kwenye matangazo au vyombo vya habari, na watafanya hivyo wakizingatia kanuni husika za kuwaajiri watoto.

Ajira ya Lazima: Wasambazaji hawatatumia ajira ya lazima, ikiwemo, bali sio tu, ajira ambapo umemfungia mtu, ajira ya utumwa au ya kumfunga mtu. Wasambazaji watatumia mbinu za kuhakikisha kwamba viwanda au makampuni hayatumiki kwa ulanguzi wa watu na watafuatilia na kuchunguza usambazaji wao ili kutambua iwapo kuna vitendo kama hivyo.

Kusumbuliwa au Kunyanyaswa: Wasambazaji lazima wawashughulikie wafanyakazi wote kwa heshima na adabu. Wasambazaji wataweka taratibu ambazo zinahakikisha kwamba hakuna mfanyakazi yeyote ambaye anasumbuliwa au kunyanyaswa kimwili, kingono, kiakili au kwa matamshi.

Kutobaguliwa: Wasambazaji hawatabagua vyovyote vile kazini iwe ni wakati wa kuajiri, kulipa/kufidia, kupandisha cheo, kuadhibu, kufuta kazi au kustaafu, kwa misingi ya jinsia, rangi, dini, umri, ulemavu, hisia za kimapenzi, nchi asilia, uanachama, msimamo wa kisiasa, kundi la kijamii, au asili.

Saa za Kufanya Kazi: Wasambazaji hawatahitaji wafanyakazi wafanye kazi zaidi ya saa za kawaida na za ovataimu zinazoruhusiwa na sheria husika. Hakuna wakati wowote ambapo mfanyakazi atafanya kazi zaidi ya saa 48 katika wiki - saa za kawaida, na wafanyakazi wataruhusiwa wapumzike kwa saa 24 mfululizo katika wiki. Wafanyakazi watafanya kazi ovataimu wakitaka. Wasambazaji hawatataka wafanyakazi wafanye kazi ovataimu mara kwa mara na watalipia ovataimu inavyostahili. Isipokuwa katika hali za kipekee, jumla ya saa za kawaida na za ovataimu katika wiki haitazidi saa 60.

Fidia/Malipo: Kila mfanyakazi ana haki ya kulipwa kwa kazi aliyofanya katika wiki, na malipo hayo yawe yanayotosha kutimiza mahitaji ya kimsingi ya mfanyakazi huyu na abakishe kiwango fulani baada ya kulipia mahitaji ya kimsingi. Wasambazaji watalipa angalau malipo ya chini zaidi yanayoruhusiwa au malipo yanayofaa kwa saa, yoyote iliyo kubwa, na watafuata mahitaji yote ya kisheria ya kimalipo, na watatoa marupurupu yoyote yanayohitajika kisheria. Wakati ambapo malipo hayatimizi mahitaji ya kimsingi ya mfanyakazi na kumbakishia kiwango fulani baada ya kulipia mahitaji ya kimsingi, Wasambazaji watachukua hatua zifaazo zinazonuia kufikisha malipo katika kiwango kinachofaa.

Uhuru wa Kushirikiana na Majadiliano ya Pamoja: Wasambazaji lazima watambue na kuheshimu haki za wafanyakazi za majadiliano ya pamoja na uhuru wa kushirikiana.

INAYOZINGATIA-DUNIA

Wasambazaji wataanzisha na kutumia mbinu za kuzuia madhara ya shughuli zao kwa mazingira. Kumaanisha kwamba, hii inahitaji kwamba Wasambazaji wafuate sheria zote husika za ndani na kimataifa zinazolinda mazingira, ikiwemo kuhifadhi vitu na kutupa vifaa hatari ipasavyo, na wajitahidi kuendesha biashara kwa njia inayopunguza utumiaji wa nishati na takataka/uharibifu, inayohimiza utumiaji wa rasilimali asilia, na inayozidisha utumiaji tena.

UHAKIKA WA BIDHAA

Kufuata Sheria: Pamoja na kutimiza mahitaji ya Kanuni hii ya Mwenendo, Wasambazaji watafuata sheria, kanuni, na mapatano mengine yote yanayotumika katika shughuli ama kazi zao.

Maadili ya Biashara: Ufisadi, unyang'anyi, ubadhirifu au uwasilishaji potofu wa bidhaa au vyanzo vya nyenzo na Wasambazaji, kwa njia yoyote, ni marufuku kabisa. Marufuku haya yanajumuisha, lakini sio tu, kutoa au kupokea rushwa ili kubadilishana na manufaa yasiyostahili au yasiyofaa na kushindwa kufichua vyanzo vya mali ghafi baada ya kuombwa kufanya hivyo. Huenda ukiukaji wa makatazo haya ukasababisha Msambazaji afutwe kazi haraka na FOTL na achukuliwe hatua ya kisheria.

Wakandarasi wadogo: Wasambazaji hawatawatumia wakandarasi wadogo katika utengenezaji wa bidhaa au sehemu za bidhaa za FOTL bila idhini ya FOTL iliyoandikwa hapo awali na watawatumia tu baada ya mkandarasi mdogo kukubali kwa maandishi kwamba atafuata Kanuni hii ya Mwenendo.

Kufuata Sheria ya Forodha: Wasambazaji watafuata sheria zote za forodha zinazotumika na wataanzisha na kudumisha mipango inayozuia uhamishaji haramu wa bidhaa.

Usalama: Wasambazaji watadumisha taratibu za usalama ili wazuie uwekaji wa shehena ama mizigo isiyo na maelezo (k.m., mihadarati na bidhaa nyingine za magendo) kwenye shehena yenye bidhaa za FOTL, ikiwemo, bali sio tu, kufuata masharti ya Ushirikiano kati ya Biashara na Forodha Dhidi ya Ugaidi (C-TPAT) ya usafirishaji nchini Marekani.

UFANYAJI NA UTEKELEZAJI

Masharti ya Kuchapisha: Wasambazaji watachapisha Kanuni hii ya Maadili katika eneo wazi linaloweza kufikiwa na wafanyakazi na wageni wote katika lugha zinazoeleweka na kila mfanyakazi, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wahamiaji wa kigeni. Msambazaji atawasiliana na kuwafunza wafanyakazi wote kila mwaka kuhusu vipengele vya Kanuni hii ya Mwenendo.

Kuhifadhi Rekodi: Wasambazaji watahifadhi rekodi kamili na sahihi kuhusu kila kipengele cha kanuni hii ya Mwenendo ili kuthibitishwa ikiwa kanuni inafuatwa.

Miongozo ya Wasambazaji; Mwongozo wa Uzingatiaji Jamii wa Mwenye Leseni: Inapohitajika, Wasambazaji watatii masharti yaliyoelezwa katika Miongozo ya Wasambazaji na/au Mwongozo wa Uzingatiaji Jamii wa Mwenye Leseni, ambao unaweza kupatikana kwenye tovuti ya shirika ya FOTL www.fotlinc.com.

Tathmini na Hatua ya Kurekebisha: FOTL hutumia wakaguzi wa ndani, pamoja na wakaguzi huru, kufanya tathmini katika eneo la kazi na/au mtandaoni ili kuhakikisha utiifu wa Kanuni hii ya Maadili. Wasambazaji watafanya kikamilifu tathmini zote kama hizi na wataandika rekodi ya ufuataji wa kanuni yenye maelezo kamili ambazo zinaweza kupitiwa upya. Wasambazaji watashirikiana na FOTL ili waunde adhabu mbalimbali zitakazoshughulikia ukiukaji kwa njia inayofaa.

Kuripoti Ukiukaji: Ili kuripoti ukiukaji unaoshukiwa wa Kanuni hii ya Maadili, wasiliana na Idara ya Wajibu wa Biashara kwa Jamii ya FOTL kwa simu katika nambari +1-270-935-2588, kwa barua pepe katika code@fotlinc.com, au kwa kuchanganua msimbo ulio upande wa kulia kwa kutumia kifaa cha mkononi. Tafadhali toa taarifa ya kina kuhusu wahusika na madai ya ukiukaji, hatua zilizochukuliwa ili kutatua suala hilo moja kwa moja, na maelezo ya mawasiliano ili tuwasiliane kwa siri kuhusu suala hilo. Tunapiga marufuku kulipiza kisasi dhidi ya watu wanaoripoti ukiukaji wa Kanuni hii ya Mwenendo au wanaosaidia au kushiriki kwa njia yoyote katika uchunguzi wa ukiukaji wa Kanuni hii ya Mwenendo ambao huenda upo. Ulipizaji wowote wa kisasi unapaswa kuripotiwa kwa FOTL kama ilivyoelezwa hapa juu.

Ilirekebishwa Februari 2022